**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS-TAMISEMI**

**Namba za simu:**
**Mkuu wa shule 0782012081/0768495193**
**Makamu Mkuu wa Shule 0765559951**
**Matron 0769773770 / 0769311586**

**Shule ya sekondari ya wasichana songe**
**S. L. P 1440**
**Musoma**
**Tarehe 16/12/2019**

**Ndugu Mzazi/Mlezi wa**…………………………………………………

………………………………………………………………………………

**S.L.P** …………………………………………………………………


………………………………………………………………………………

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA SONGE HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA MKOA WA MARA MWAKA 2020**

1.Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Kwanza katika shule hii mwaka 2020. Shule ya Sekondari ya wasichana Songe ipo umbali wa Kilometa 7 Mashariki mwa mji wa Musoma, na Mita 400 kutoka barabara kuu iendayo Mwanza. Usafiri wa daladala kutoka mjini au stendi ya mabasi ya Mikoani Bweri unapatikana katika vituo vya stendi za daladala za mjini na Bweri kwa nauli ya shilingi 400/=.

Muhula wa masomo utaanza terehe 06/01/2020 Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 06/01/2020 Mwisho wa kuripoti ni tarehe 24/01/2020.

Karibu sana Songe Sekondari.



**MKUU WA SHULE**

1. **Mambo ya kuzingatia:-**

**1.1 Sare ya shule**

(a) Sare ya shule hii ni sketi ndefu mbili (2) za rangi ya ( light blue) bluu bahari Kitambaa kizito zenye marinda ya kawaida zinazofika kwenye kisigino (na sio linda box) pamoja na mashati mawili (2) meupe mikono mifupi.
(b) Kwa waislamu rangi ya kijuba ifanane na rangi ya sketi.
(c) Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.

(d) Sare ya michezo kwa shule hii ni Bukta na T-shirt za rangi ya dark blue na raba nyeusi
(e) Soksi jozi mbili nyeupe zisizo na alama yoyote
(f) Sweta ya rangi ya blue yenye alama ya ''V'' shingoni.
(g) Nguo za kushindia (Shamba dress) ni gauni mbili (2) za rangi ya **Pinki Zain**, Kitambaa kizito. Mshono wake ni solo ndefu inayofika kwenye kisigino, yenye mikono mifupi kama ya shati na shingo yenye **V** kifuani.
(h) Trucksuit ya rangi Nyeusi isiyo na kofia itakayovaliwa usiku wakati wa kujisomea.
(i) Huruhusiwi kusuka. Unatakiwa kuwa na nywele fupi
(j) Mapambo ya aina yoyote hayaruhusiwi (mfano, kupaka rangi, kuvaa hereni, bangiri nk).

**2.2 Mahitaji muhimu ya mwanafunzi**

i. Godoro la Sponge la 3 ft kwa 6ft
ii. Mashuka mawili rangi ya light blue
iii. Sanduku la bati kwa ajili ya kutunzia vifaa vyake
iv. Chandarua rangi ya blue
v. Tochi kwa tahadhari usiku umeme ukikatika
vi. Madaftari makubwa (Counterbooks) yasiyopungua kumi na mbili
vii. Kalamu za kutosha, Rula pamoja na mkebe wa hesabu
viii. Kamusi ya Kiswahili sanifu , English dictionary na Mkebe wa hesabu (**Mathematical set)**
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko, kikombe na kidumu cha kutunzia maji ya kunywa)
x. Ndoo ndogo moja na kubwa moja kwa ajili ya kufulia na kuogea
xi. Kanga au taulo au kitenge kwa ajili ya kuogea
xii. Picha nne (passport size) za rangi za mwanafunzi akiwa kwenye shati la shule. Ziwe za hivi karibuni.
xiii. Mfagio mmoja wa chelewa kwa usafi wa mazingira yako

**NB:** Kwa kuwa mwanafunzi haruhusiwi kuja na simu shuleni, mzazi unatakiwa kutumia simu ya shule namba: **(0757 360 529)** kwa ajili ya mawasiliano pamoja na kutuma fedha kwa ajili ya matumizi ya mwanao. Unapotuma pesa **tuma na ujumbe mfupi ukitaja jina la mwanafunzi na kiasi ulichotuma.**

## 3.0 **Sheria na kanuni Muhimu za shule hii**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu ya Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na mafunzo ya ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na uendeshaji Elimu.

### 3.1 Mambo muhimu ya kuzingatia

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya darasa kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa;
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote; na
i) Kutunza mali za umma.

### 3.2 Makosa Yafuatayo Yanaweza Kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa Shule

i. Wizi
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
iii. Kugoma au kuhamasisha mgomo
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/ walezi na jamii kwa ujumla
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yoyote yule
vi. Kufuga nywele ndefu au kunyoa mtindo usiokubalika
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
viii. Uvutaji wa sigara
ix. Uasherati, uhusiano wa jinsia moja au kuolewa
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi
xii. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni uwapo shuleni
xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule
xiv. Kudharau Bendera ya Taifa
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k
xvi. Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi
xvii. Kukataa adhabu kwa makusudi
xviii. Ubakaji

**4.0 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi**

a) Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni, na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule
d) Picha za Wazazi na Ndugu wawili wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu (Picha zibandikwe kwenye Jedwali husika
e) Pia mwanafunzi ajapo shuleni ni muhimu aje na vitu vifuatavyo:
    i. Kivuli (Photocopy) cha cheti cha kuzaliwa kinachotolewa na Serikali (Birth Certificate)
    ii. Kadi ya Bima ya afya (kama anayo) NHIF

NB. Tafadhali soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA SONGE SEKONDARI**

**Saini ya Mkuu wa Shule ..........................................**

**Jina la Mkuu wa Shule ROSEMARY B. JOHN**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ........................................**

**SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA SONGE**

**FOMU YA MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI PAMOJA NA AHADI YA UTII WA SHERIA ZA SHULE**

1. Jina kamili (Kama ilivyo kwenye TSM9) ……………………………………………………….
2. Anwani ya nyumbani …………………………………………………………………………..
3. Tarehe ya kuzaliwa …………………
4. Mahali ulipozaliwa, Kijiji/Mtaa …………………………..
   Kata……………………………...Tarafa……………..
   Wilaya………………………...Mkoa……………………………..
5. Mahali unapoishi kwa sasa ………………………………………..
6. Shule ya msingi ulikotoka…………………………………………………………………. Anwani (**Muhimu sana**) ……………………………………………
7. Dini/Dhehebu…………………………………………………………..
8. Kabila………………………………………………………………………..
9. Taifa (Mtanzania/Si Mtanzania)………………………………………………..
10. Baba na Mama wanaishi au hawaishi? (a) Baba ………………. (b) Mama ………………..
11. Baba na mama pamoja na jamaa wengine wawili ambao wanaweza kupelekewa taarifa zako muhimu kwa masuala ya shule:

| NA | JINA | PICHA | UHUSIANO | KAZI | ANUANI | NAMBA YA SIMU |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | | | |
| 2 | | | | | | |
| 3 | | | | | | |
| 4 | | | | | | |

NB:Siku ya wazazi inayoruhusiwa wanafunzi kutembelewa ni **JUMAPILI YA KWANZA** miezi ya: **Machi,** na **Agosti** tu**.** Wazazi/Walezi watakaoruhusiwa kuwaona wanafunzi ni wale walioorodheshwa kwenye jedwali tu.

12. **Ahadi ya utii:**

(a) Mimi (Mwanafunzi)……………………………………….nathibitisha kuwa taarifa nilizozijaza hapo juu ni za kweli. Ahadi yangu, Nakubali kwa dhati kabisa nafasi niliyopewa na Taifa kujiunga na shule hii na ninaahidi kufuata sheria na taratibu zote za shule kama zilivyotolewa na zitakavyotolewa na uongozi wa shule.

…………… ……………**.**

Sahihi ya Mwanafunzi Tarehe

(b) Mimi (Jina la Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi)…………………………………………………………**..** ambaye ni Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi ……………………………………………… nimeyasoma masharti na sheria za shule ya Sekondari Songe ambako binti yangu amechaguliwa kujiunga. Naahidi kwamba nitamuhimiza mwanangu kufuata sheria na taratibu zote za shule kama zilivyoelezwa na kumtimizia mahitaji yake ya shule. Aidha naahidi kushirikiana na uongozi katika malezi bora ya mwanangu ili baadaye awe raia bora na mwema wa Taifa letu.

…………………… ……………………

Sahihi ya Mzazi/Mlezi Tarehe


**SONGE SECONDARY SCHOOL**
**MEDICAL EXAMINATION FORM**

**SONGE SECONDARY SCHOOL,**
**P.O.Box 1440,**
**MUSOMA.**
**DATE…………………**

**To Medical Officer,**
**………………………………………**

**………………………………………**

**Ref……………………………………………………………..**
**(NAME OF STUDENT)**
Please examine the above named Student as per Medical examination form below,



**HEADMISTRESS**
**MEDICAL EXAMINATION FORM**
(To be completed by Government Medical Officer)

Full Name…………………………………………………………………………………………..

Age………………Height……………… (cm)  Weight………………… (Kg)

1. Blood count (Red and White)………………………………………………………………..
2. Stool Examination……………………………………………………………………………
3. Urinary analysis……………………………………………………………………………….
4. STDs and other V.D……………………………………………………………………………
5. T.B and Leprosy test………………………………………………………………………......
6. Eye test……………………………………………………………………………………………
7. Ear test……………………………………………………………………………………………
8. Chest ………………………………………………………………………………………………
9. Abdominal test………………………………………………………………………………..
10. Blood Group **(Very Crucial)**…………………………………………………………………
11. Spleen………………………………………………………………………………………………
12. Pregnancy test………………………………………………………………………………..
13. Bilharzias ………………………………………………………………………………………..
14. Asthma……………………………………………………………………………………………
15. Skin diseases……………………………………………………………………………………..
16. Any additional defects or impairments, infections, chronic or family diseases (e.g. Sickle cell),

…………………………………………………………………………………………………………………………
I have examined the above named student and I certify that she is FIT/NOT FIT to pursue Secondary Education.
Signature…………………………………………Date……………………………..
Station……………………………………………………………………………………
Designation and Official Stamp……………………………………………………